USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

Rukwa Sustainable Development
Organization RUSUDEO

LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)
SHERIA NA ULINZI WA MAZINGIRA

USIMAMIZI ENDELEVU WA MALIASILI

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za maliasili. Maji, misitu, wanyamapori na madini ni sehemu ya tunu zipatikanazo nchini Tanzania. Pamoja na mambo mengine, rasilimali hizi ni muhimu kiuchumi, kijamii na kimazingira. Kimahususi, rasilimali hizi hutambulisha Tanzania mbele ya mataifa mengine. Uwepo wa Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu zaidi Afrika, Ziwa Tanganyika lenye kina kirefu zaidi Afrika na Ziwa Victoria, ambalo ni ziwa kubwa zaidi Afrika ni sehemu ya utajiri adhimu wa nchi ya Tanzania.

Benki Kuu ya Tanzania kupitia ripoti zake inataja mchango mkubwa wa Maliasili kwa uchumi wa Tanzania. Sambamba na ripoti ya Benki kuu, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia majukwaa mbalimbali inaonesha mchango wa Maliasili kwa uchumi wa Tanzania. Mamlaka zote mbili yaani Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Maliasili na Utalii zinaripoti juu ya maliasili kuchangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa (GDP) na asilimia 25 ya fedha za kigeni.

Aidha, Tanzania inayotambuliwa kama Ardhi ya Serengeti, Kilimanjaro na Zanzibar ni bandari ya wanyamapori wengi wanaoishi katika Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Tanzania ina misitu ya asili na misitu ya kupandwa. Tanzania ni tajiri wa rasilimali maji. Bahari ya Hindi ipatikanayo Mashariki mwa nchi, mabonde 9 ya maji, maziwa, mito na vijito ni vyanzo thabiti vya maji na hutunza mimea na viumbe maji ambavyo ni chanzo cha protini kwa watu waishio pembezoni mwa vyanzo husika.

Madini ni rasilimali nyingine muhimu kwa nchi. Kiupekee kabisa Tanzania ndio chanzo pekee cha madini ya Tanzanite. Upatikanaji wa mawe matatu makubwa yenye uzito tofauti yaliyotokea hivi karibuni huko Simanjiro Manyara ni sehemu nyingine ya sifa nzuri ya nchi ya Tanzania. Sambamba na Tanzanite, Tanzania pia ina madini ya dhahabu, almasi, pamoja na madini mengine ya ujenzi. Kusini mwa Tanzania yaani Mtwara na Lindi ni bandari ya gesi asilia ambayo kwa sasa inaendelea kuvunwa na kutumika katika utengenezaji wa umeme.

Sifa juu ya utajiri wa Tanzania ni nyingi. Ikumbukwe pia Tanzania inahodhi turadhi sita za dunia (Serengeti, Ngorongoro, Mji Mkongwe, Kondoa, Iringa, Selous). Haya na mengine mengi ni sehemu muhimu ya utajiri wa Tanzania na huchagiza upatikanaji wa faida za kifedha kwa nchi.

Mkoa wa Rukwa upatikanao magharibi mwa Tanzania nayo ni sehemu yenye tunu nyingi za Maliasili. Uwepo wa Ziwa Rukwa, maporomoko ya Kalambo, wanyamapori ndani na nje ya Mapori ya Rukwa na Lukwati, Pori tengefu la Uwanda ambalo limechukua asilimia 80 ya ziwa Rukwa, misitu, na ardhi yenye rutuba tena inayovuta wawekezaji toka sehemu mbalimbali za

nchi ni sehemu ya utajiri wa mkoa huu. Utajiri wa mkoa wa Rukwa kama ilivyo kwa maeneo mengine ya Tanzania hutoa fursa kwa wananchi kunufaika kiuchumi, kimazingira na kijamii.

Usimamizi Endelevu wa Maliasili ni Mradi mtambuka wa miaka mitano (2020-2025) unaolenga kuimarisha Usimamizi Endelevu wa Maliasili Mkoani Rukwa katika Wilaya za Sumbawanga na Nkasi. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Watu wa Marekani. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili unaotekelezwa na Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo Endelevu yaani RUSUDEO unatambua utajiri wa Rukwa. Kimahususi kabisa mradi unatambua uwepo na umuhimu wa rasilimali za Maliasili zinazopatikana katika milima ya Lyamba lya Mfipa.

Utajiri wa eneo hili ulithibitishwa na LEAT na RUSUDEO kupitia utambulishaji na tathimini ya mradi iliyofanyika kati ya tarehe 13-06-2020 hadi tarehe 24-06-2020. Ukusanyaji wa taarifa katika tarafa za Chala, Kate na Mtowisa, kata za Nkandasi, Mkwamba, Kipande, Muze, Kalumbaleza na mwadui na vijiji 15 vya mradi ulitosha kudhihirisha ukubwa, umuhimu na hali za usimamizi wa maji, misitu, wanyamapori na ardhi. Itoshe kusema wakazi waishio sambamba na milima na misitu ya Lyamba lya Mfipa hutegemea maliasili kukidhi mahitaji yao ya kimaisha. Maji ni muhimu nyumbani, kwa kilimo na unyweshaji wa mifugo. Ardhi ni msingi mkuu wa shughuli za kiuchumi kwa jamii kwani hutoa fursa kwa wakazi kuendesha kilimo na ufugaji. Kadhalika, bayoanuai huboresha uwiano wa ki-ikolojia.

Pamoja na faida lukuki za ardhi, misitu, wanyamapori na maji bado usimamizi wa rasilimali hizi unazungukwa na changamoto nyingi hivyo kufifisha fursa za wananchi na ustawi wa rasilimali. Vyanzo vya maji, kwa mfano, vinaendelea kuvamiwa na shughuli za kilimo na ufugaji, ongezeko la sumu na vimelea vya magonjwa na mmomonyoko wa udongo. Kuvunjika kwa madaraja tarafa ya Mtowisa ni kielelezo tosha cha namna Mabadiliko ya Tabianchi na uvunaji usiofuata taratibu ulivyo mbaya kwa ustawi wa watu na ulinzi wa mali zao. Kama vile haitoshi, wakazi wa vijiji hususani ukanda wa chini wa Lyamba lya Mfipa hushambuliwa na maradhi ya matumbo kutokana na kuchafuliwa kwa vyanzo vya maji.

Ni kwa muktadha huu LEAT na mshirika wake RUSUDEO inatekeleza mradi huu wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili kama mkakati wa kuelekea katika usimamizi thabiti wa rasilimali za maliasili. LEAT na RUSUDEO tunaamini uwazi, uwajibikaji, utawala wa sheria na ushiriki wa wananchi katika kutunza rasilimali ni mwanzo wa kuongeza ustahimilivu wa jamii. Timu ya utekelezaji wa mradi inaamini ili kufikia utawala bora wa maliasili lazima jamii iwezeshwe ki-ufahamu na ki-zana (tools). Hivyo elimu kwa wadau, kusaidia kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi, kusaidia kuboresha uelewa na ufahamu wa kamati mbalimbali, kuratibu utengenezwaji wa sheria ndogo, upandaji miti, kufanya kazi na vikundi vya kijasiriamali ni jitihada ya kuelekea katika jamii yenye usimamizi madhubuti wa maliasili kwa kuzingatia upatikanaji wa haki za msingi za binadamu na viumbe.

Vijiji vya Mradi

Wilaya	Tarafa	Kata	Kijiji
Sumbawanga	Mtowisa	Muze	1. Ilanga
			2. Mbwilo
			3. Kizungu
		Kalumbaleza	4. Kalumbaleza
			5. Mnazi Mmoja
		Mwadui	6. Mtapenda
			7. Nkwilo
			8. Mpete
Nkasi	Chala	Nkandasi	9. Kisula
			10. Malongwe
		Mkwamba	11. Lyele
			12. Tambaruka
			13. Swaila
			14. Itindi
	Kate	Kipande	15. Nkomolo II (Chamiku)

RAMANI YA ENEO LA MRADI



SHUGHULI ZA MRADI

Mradi huu unalenga kuboresha usimamizi wa maliasili. Kimahususi, mradi utajikita kuboresha usimamizi wa **ardhi**, **maji**, **misitu** na **wanyamapori**. Ili kufikia lengo kuu, utekelezaji wa mradi umegawanya matokeo ya kati ya mradi (Intermediate Results) katika maeneo makuu manne. Aidha, kila tokeo la kati limetengenezewa shughuli mahususi ambazo kutekelezwa kwake kutahakikisha ufikiaji wa matokeo.

Tokeo la kati la 1: ***Kusaidia utengenezaji na utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Ardhi, Sheria ndogo na zana nyinginezo ili kusaidia usimamizi na utawala wa rasilimali za maliasili.***

Shughuli:

1.1.1 Kuwezesha utengenezaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi wa Ardhi ili kuboresha usimamizi na utawala wa rasilimali za maliasili.

1.1.2 Kuratibu utolewaji wa Hati Miliki za Kimila kwa ajili ya usimamizi wa maliasili na usalama wa ardhi.

1.1.3 Kuwezesha wanavijiji kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kuboresha usimamizi wa ardhi na rasilimali za maliasili.

Tokeo la kati la 2: ***Kuboresha uwezo wa jamii kuhoji taasisi zilizopewa jukumu la kusimamia rasilimali za maliasili ili kuboresha uwajibikaji.***

Shughuli

2.1.1 Mafunzo ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (UJJ) kwa Halmashauri za Vijiji, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kamati za Usimamizi wa Maliasili, na wanavijiji wenye ushawishi.

2.1.2 Mafunzo ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii kwa Maafisa 26 wenye dhamana na usimamizi wa mazingira na maliasili katika ngazi za halmashauri za wilaya.

2.1.3 Mafunzo ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii kwa wajumbe 40 wa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata.

2.1.4 Mafunzo ya kujengea uwezo wafanyakazi watano (5) wa RUSUDEO, Maafisa ngazi ya tarafa (3), kata (Waratibu Elimu wa Kata 5, Maafisa Watendaji wa Kata, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata) na Maafisa tarafa 2 juu ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii.

2.1.5 Warsha ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (UUJ) kwa madiwani 73 wanaowakilisha kata zilizopo Halmashauri za Nkasi na Sumbawanga.

2.1.6 Warsha ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii kwa wajumbe 40 wa Jumuiya za Watumia Maji (WUA) na wajumbe 105 wa COWSO.

2.1.7 Mafunzo kwa wanakijiji 600 juu ya Uwajibikaji wa Uwajibikaji wa Jamii.

2.1.8 Kuendesha mikutano 30 ya uhamasishaji jamii (15 shuleni na 15 maeneneo ya umma) juu ya Uwajibikaji wa Uwajibikaji wa Jamii kwa njia ya vikundi vya sanaa.

2.1.9 Kuwezesha/kuratibu uanzishwaji na ufundishaji wa Kamati 15 za Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii ngazi za vijiji.

2.1.10 Kuziwezesha Kamati za Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii (UJJ/SAM) za vijiji kutoa mirejesho ya matokeo ya shughuli zao kwa watumishi wa serikali.

Tokeo la Kati la 3: *Kuboresha kwa uwezo wa jamii na mamlaka za wilaya na vijiji kusimamia rasilimali za maliasili.*

Shughuli

3.1.1 Mafunzo ya kujenga uwezo kwa Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Ardhi za Vijiji, Kamati za Maliasili za Vijiji na wanakijiji wenye ushawishi kwenye usimamizi na utawala wa maliasili.

3.1.2 Mafunzo ya kuboresha uwezo juu ya usimamizi na utawala wa rasilimali za maliasili kwa maafisa 26 ngazi ya wilaya (wenye dhamana na usimamizi wa maliasili na mazingira).

3.1.3 Mafunzo ya kujenga uwezo juu ya usimamizi wa maliasili kwa wajumbe 40 wa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata.

3.1.4 Mafunzo ya kuboresha uwezo kwa ngazi za tarafa na kata (Maafisa tarafa 3, Waratibu Elimu 5, Maafisa Watendaji 5, Maafisa Maendeleo ya Jamii 5) na maafisa tarafa watatu (3).

3.1.5 Warsha juu ya usimamizi wa maliasili kwa madiwani toka kata 66 za Sumbawanga na Nkasi.

3.1.6 Warsha ya usimamizi wa maliasili kwa wajumbe 40 wa WUA na wajumbe 105 wa COWSO

3.1.7 Mafunzo kwa wanakijiji 600 juu ya usimamizi na utawala wa maliasili.

3.1.8 Kuendesha mikutano 15 ya uhamasishaji jamii (15 shuleni na 15 maeneo ya umma) juu ya Mabadiliko ya Tabianchi, usimamizi wa maliasli na utawala kwenye kila kijiji kwa njia ya Vikundi vya Sanaa.

3.1.9 Kusaidia vikundi vya kijamii vya uzalishaji mali na kujitafutia kipato vyenye kufanya shughuli zinazotilia maanani uendelevu wa mazingira.

3.1.10 Mafunzo kwa wanavijiji juu ya shughuli za uzalishaji mali na ujasiriamali.

3.1.11 Kuwezesha jamii kulinda na kuhifadhi rasilimali za maliasili kupitia upandaji miti kama zana ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi kwa kupanda miti 400,000.

3.1.12 Kuwezesha wanajamii 225 kutengenza na kutumia majiko banifu.

Tokeo la Kati la 4: *Kuongeza uelewa kwa jamii kwenye maswala ya usimamizi wa maliasili, mabadiliko ya tabia nchi na ufuatiliaji wa uwajibikaji jamii kwa kutumia machapisho, sanaa na vipindi vya redio.*

Shughuli

4.1.1 Ufuatiliaji na utunzaji wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za mradi

4.1.2 Kuwezesha vikundi vya sanaa kuandaa na kufikisha jumbe mbalimbali kwa jamii zihusuzo usimamizi endelevu wa maliasili, ufuatiliaji wa uwajibikaji jamii, mabadiliko ya tabia nchi na mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa njia ya maigizo.

4.1.3 Kutengeneza na kusambaza makala za gazeti.

4.1.4 Kuandaa na kurusha vipindi vya televisheni na radio.

4.1.5 Kuandaa na kuchapa miongozo ya mafunzo juu ya usimamizi wa maliasili (misitu, wanyamapori, na maji), utawala wa ardhi na Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii.

4.1.6 Kuandaa na kuchapa vipeperushi vyenye ujumbe juu ya usimamizi endelevu wa maliasili, mabadiliko ya tabianchi, utawala wa ardhi na Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Jamii.